**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MTERA DAM

**May, 2024**

**MPWAPWA-Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Shule ya Sekondari **MTERA DAM**

S.L.P 92

**MPWAPWA**

25/05/2024

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**

**………………………………..………….**

**S.L.P ……………………………………..**

**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MTERA DAM HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA MKOA WA DODOMA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya HGL

Shule ya Sekondari **MTERA DAM** ipo barabara kuu ya Dodoma - Iringa umbali wa Kilometa 136 kutoka DODOMA, na Kilometa 120 kutoka IRINGA. Usafiri wa basi kutoka DODOMA mjini unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi cha Mkoa (NANENANE) au Kikuyu (Magorofani) kila siku. Kwa wanaotokea mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Iringa na Songwe panda magari yaendayo Dodoma na ushuke kituo cha MTERA STAFF (Dodoma Gate). Aidha kwa wanaotokea mikoa ya Kaskazini, Magharibi na kanda ya Ziwa utapanda magari yaendayo Iringa, Mbeya au Songea na kushukia MTERA STAFF (Dodoma Gate). Hapo utachukua pikipiki kuja shuleni kwa Sh. 1,000/= tu.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe………………….., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe…………………….

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule ni sketi mbili ndefu rangi ya DARK BLUE nzito ya kuiva zenye mshono wa V mbele
ii. Mashati meupe mawili ya mikono mirefu
iii. Sare ya Michezo Track Suit ya rangi ya LIGHT BLUE na raba nyeupe
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeupe
vi. Hijab nyeupe
vii. Sweta la rangi ya KIJIVU
viii. Nguo za kushindia ni T Shirt ya Kijivu yenye kola isiyo na maandishi na Sketi NYEUSI.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari ya counter book tisa (Quire 4)
ii. Karatasi A4 Ream 2 kwa mwaka
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika orodha iliyopo hapo chini;
iv. Scientific Calculator
v. Godoro lenye ukubwa wa futi mbili na nusu upana na futi sita urefu pamoja na mto wa kulalia
vi. Mashuka Jozi 2 (jozi moja rangi ya light bluu na nyingine rangi ya pinki), blanket nyepesi 1 na chandarua nyeupe
vii. Nguo za ndani za kutosha
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko
x. Kwanja 1, jembe lenye mpini, mopa 1, mifagio 2 (wa ndani na nje)
xi. Sanduku imara au trunker la kuhifadhia mali yake kwa usalama bwenini
xii. T-shirt ya shule na tai zinapatikana shuleni

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 70,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**ANGALIZO**

**Michango yote iwekwe kwenye akaunti ya shule namba 50401100046 (MTERA DAM SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION ACCOUNT)**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na**

i. Wizi
ii. Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
vii. Uvutaji wa sigara;
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, au kuolewa;
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiii. Kudharau Bendera ya Taifa;
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

**i.** Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
**ii.** Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
**iii.** Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
**iv.** Picha ndogo (Pasport Size) moja kwa kila mzazi na ndugu watatu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MTERA DAM**

......................

**Lutengano H. Mwalubandu**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MTERA DAM
S. L. P. 92
MPWAPWA

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule 0755711683
- Makamu Mkuu wa Shule 0755248561
- Mwandamizi Taaluma 0755296055
- Matron 0764878608

**ORODHA YA VITABU MUHIMU ANAVYOPASWA MWANAFUNZI KUJA NAVYO**

**ENGLISH**

1. Ashel, N (2009), Advanced level English a practical approach. DSM.
2. Advanced English language, Form five & six by Oxford
3. Ashel, N (2011), Advanced level literature. The essential guide, good book publishers, DSM.
4. English language for Secondary Schools, literature and stylistic form five and Six (TIE) Paper 2

**HISTORY**

1. July, R.W.(1992).A history of the African people, East African Educational Publishers Nairobi Kenya.
2. Rodney. (1976).How Europe underdeveloped Africa, Publishing House, DSM, Tanzania.
3. History of secondary schools: Form five (TIE).
4. Nelson Throne Essential Modern World History(Oxford)
5. The History of Modern World(2007) 6th Edition by Oxford University Press

**GEOGRAPHY**

1. (Collin Buckle), Land Form in Africa.
2. C. R. Kothari, Research Methodology.
3. (H. C. Truran),A Practical Guide to Statistical Maps and Diagrams
4. Practical Geography Alive by Zizti
5. Map Reading, photography interpretation, field Research, Statistics and Survey illustrated by Ellias Anthony Mkoko
6. Affordable Edition for Secondary and High School learners kot Publishers
7. A comprehensive approach to physical geography by DT Msabila
8. Human and Economica Geography by Gillan C. Morgan
9. Soil and Climatology by Zisti

**GENERAL STUDIES**

1. Richard, R. F. Mbalase. General studies for Advanced level Certificate.
2. Mgaywa B. M. General Studies for Advanced level 3rd Edition.
3. Joanes BigirwaMungu & Sospeter M.D, Understanding Advanced level General Studies.

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**FROM THE HEADMASTER MTERA DAM SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 92, MPWAPWA**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

**NAME OF STUDENT………………………………………….AGE………..**

MEDICAL HISTORY

| | **YES** | **NO** |
|---|---|---|
| Tuberculosis | | |
| Asthma | | |
| Heart disease | | |
| Jaundice | | |
| Peptic ulcers | | |
| Epilepsy | | |
| Diabetes mellitus | | |
| Kidney problem | | |
| Anaemia | | |
| Neurosis | | |

**PHYSICAL EXAMINATION:**

- Respiratory System
- Cardiovascular system-
- Gastrointestinal system-
- Urinary system-
- Reproductive system-
- Eye: R:-
  L:-
  E.N.T-

INVESTIGATION

1. Blood -HB…………………………….. -WBC…………….……………….
   -ESR………………………….…. -VDRL Test…….…………………...
2. Urine-
   Pregnancy………………………………Sed……………………………………..

I have examined the above student and considered that she is physically and mentally fit/ not physically and mentally fit for further studies.

Signature……………………………………. Designation……………………….
Station……………………………………... Date………………………………

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MTERA DAM**

A. Mimi mwanafunzi…………………………………………………… (majina matatu) wa SLP;……………………..nimesoma maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari MTERA DAM pamoja na sheria na Kanuni zake. Nimeelewa vema, naahidi kuwa mtiifu na mwaminifu wakati wote nitakapokuwa shuleni na mahali pengine popote. Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu wote na nisome kwa bidii ili nipate elimu bora. Nitakuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa ajili ya maendeleo yangu ya Shule na Taifa zima kwa ujumla.

Sahihi……………………………… tarehe…………………………

B. Mimi…………………………………………………………..Mzazi/Mlezi

........................................................................................................... wa mwanafunzi:

........................................................................................................... nimesoma maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari MTERA DAM pamoja na sheria na kanuni za shule. Naahidi nitamsaidia mwanafunzi huyukwa hali na mali ili aweze kukamilisha masomo yake ya sekondari bila kipingamizi chochote.

Na nipo tayari kufikishwa kwenye vyombo vya dola endapo nitashindwa kumtimizia kijana wangu mahitaji yake ya msingi yaliyoorodheshwa kwenye barua ya kujiunga na Kidato cha Tano. Na maandishi haya yatumike kama ushahidi dhidi yangu.

Nitashirikiana na uongozi wa Shule ili kutimiza azma hii. Kama sitapatikana tafadhali wafuatao (ndugu watatu) waitwe shuleni pakitokea tatizo au kitu kingine chochote kitakachohitaji uwepo wangu.

**NDUGU WA KARIBU**

i. ………………………………………………………………………………..
Namba ya Simu……………………………………………………………….
Uhusiano wake na mwanafunzi……………………………………………

ii. ………………………………………………………………………………..
Namba ya Simu……………………………………………………………….
Uhusiano wake na mwanafunzi……………………………………………

iii. …………………………………………………………………………………
Namba ya Simu……………………………………………………………….
Uhusiano wake na mwanafunzi……………………………………………

**Uhusiano Mfano Shangazi, kaka nk